**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**DIVISHENI YA KAZI**

**ILIYOKETI DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA MAREJEO NA. 164 YA 2020**

**BAINA YA**

**SAID M. CHOKI............................................................MLETA MAOMBI**

**NA**

**DAR ES SALAAM DEVELOPMENT CORPORATION (DDC).....MJIBU MAOMBI**

# HUKUMU

Tarehe ya Amri ya Mwisho: 04/03/2021
Tarehe ya Hukumu: 07/05/2021

**A. E. MWIPOPO, J.**

Said M. Choki ambaye ni Mleta Maombi katika shauri hili la marejeo ameleta maombi haya akiomba Mahakama irekebishe uamuzi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi uliotolewa katika mgogoro wa kikazi na. CMA/DSM/ILA/12/2020 wa tarehe 8 Aprili, 2020, na Mhe. C. Kalinga, Msuluhishi. Mleta Maombi anaomba yafuatayo:-

1. Mahakama hii ikipendezwa iitishe kumbukumbu za Tume ya Usuluhishi na Uamuzi Kanda ya Dar Es Salaam iliyoketi Ilalakwa ajili ya kurekebisha mwenendo mzima na uamuzi wa Tume unaohusiana na pingamizi lililowekwa na Mjibu Maombi katika mgogoro wa kikazi na. CMA/DSM/ILA/12/2020 ambao ulitolewa tarehe 8 Aprili, 2020,

na Mhe. C. Kalinga, Mwamuzi, ili kujiridhisha kuhusu usahihi, uhalali, utaratibu na ustahili wake.

2. Baada ya kurejea uamuzi husika, Mahakama iridhie kubadilisha uamuzi wa Tume unaohusiana na pingamizi la awali na iielekeze Tume ya Usuluhishi na Uamuzi iendelee na kuamua madai ya Mleta Maombi katika mgogoro wa kazi na. CMA/DSM/ILA/12/2020 kama ulivyowasilishwa mbele ya Tume kwa kupitia fomu na. 1.
3. Amri nyingine yoyote ambayo Mahakama hii itaona inastahili kutolewa.

Historia fupi ya shauri hili ni kuwa Mleta Maombi alifungua mgogoro wa kikazi mbele ya Tume ya Usuluhishi na Uamuzi Ofisi ya Ilala kupitia fomu na. 1. Wakati shauri likiwa katika hatua ya usuluhishi (mediation) mbele ya Mhe. Kalinga, Mjibu Maombi ambaye ni Shirika la Maendeleo la Dar Es Salaam (Dar Es Salaam Development Corporation – DDC) aliweka pingamizi kuwa Tume haina mamlaka ya kusikiliza shauri husika kwa kuwa Mleta Maombi ni Mtumishi wa Umma. Tume ilikubaliana na pingamizi hilo ambapo iliona kuwa Mleta Maombi ni Mtumishi wa Umma na hivyo ikaona haina mamlaka ya kusikiliza mgogoro huo. Mleta Maombi hakuridhika na uamuzi huo wa Tume ndipo akafungua shauri hili la marejeo hapa Mahakamani.

Katika shauri hili, pande zote mbili zilikuwa zinawakilishwa ambapo Mleta Maombi anawakilishwa na Bw. George Mwiga, Wakili, na Mjibu Maombi anawakilishwa na Bw. Bahati Mabula, Wakili.

Akifanya mawasilisho ya msingi kuunga mkono maombi haya, Wakili wa Mleta Maombi alieleza kuwa anaanza kwa kuwasilisha kwa pamoja hoja ya kisheria ya kwanza, ya pili, ya saba na ya nane kama zilivyo katika aya ya nane ya kiapo cha mwombaji ambazo zinahusu Tume kukosea kisheria katika uamuzi wake kuwa Mjibu Maombi ni shirika lililopo chini ya Serikali. Mleta maombi ameeleza kuwa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi kuwa ilifanya makosa kutamka kwamba mleta maombi alifanya kazi kama Mtumishi wa Umma. Mleta maombi akitoa ushahidi wake aliieleza Tume kuwa yeye si Mtumishi wa Umma kwa mujibu wa kifungu cha 3(a) (ii) ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 98 kama ilivyorejewa mwaka 2002. Tume haikuzingatia mawasilisho haya. Utaratibu wa mishahara wa Mleta Maombi ni tofauti na utaratibu wa malipo ya watumishi wengine wa Umma ambao mishahara yao hulipwa kwa viwango vya TGS na lazima mtumishi wa Umma awe na "Check Number". Lakini mleta maombi hakuwa na hivyo vitu na alilipwa kwa utaratibu uliopangwa na Mjibu Maombi. Aidha, mishahara ya mleta maombi huwa inafanywa kwa utaratibu wa mjibu maombi na sio wa Serikali Kuu. Tume ilipuuza ushahidi wote huu katika

kufikia maamuzi yake. Haya yote yanaonyesha kuwa mleta maombi sio Mtumishi wa Umma.

Wakili wa Mleta Maombi aliendelea kuwasilisha kuwa katika kiapo kinzani (Counter Affidavit) kilichowasilishwa na Mjibu Maombi katika aya ya 5(iii)(iv)(v) na (vi) ameeleza kuwa Mjibu Maombi anamilikiwa na Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam kwa mradi. Mjibu maombi anaongozwa chini ya Bodi ya Wakurugenzi ya shirika, hata ajira ni jukumu la Bodi ya Wakurugenzi. Ni maoni ya Mleta Maombi kuwa ajira za watumishi wa Umma zinatekelezwa chini ya utaratibu wa utumishi wa Umma na si vinginevyo. Hivyo, kwa ajira ya mleta maombi kuwa chini ya Bodi ya Wakurugenzi kunamuondoa kuwa Mtumishi wa Umma. Mleta Maombi anaeleza kuwa hakuwahi kuwa Mtumishi wa Umma, suala kama hili lilifanyiwa tafsiri na Mahakama hii katika kesi ya **Jeremiah Mwandi dhidi ya Shirika la Posta Tanzania,** marejeo ya kazi Na. 6 ya 2019, Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi, iliyoketi Kigoma (haijaripotiwa) ambapo Mahakama ilieleza kuwa mtumishi wa Shirika la Posta hakuwa Mtumishi wa Umma.

Aidha, suala la madai dhidi ya mjibu maombi kupelekwa mbele ya Tume ya Usuluhishi na Uamuzi sio la kwanza. Mahakama hii ilitolea uamuzi katika kesi ya **Floriana Kinawiro dhidi ya Shirika la Maendeleo Dar es salaam**, marejeo Na. 285 ya 2019, Mahakama kuu

Divisheni ya Kazi, Dar es Salaam, (haijaripotiwa), ambapo si Mahakama hii au wadaawa waliwasilisha pingamizi kuwa mleta maombi katika shauri hilo kuwa hakuwa mtumishi wa Umma. Tunaamini shauri hili litasaidia Mahakama kufikia maamuzi ya haki.

Mleta Maombi aliomba kuwasilisha hoja za kisheria za marejeo haya namba "iii" na "v" kama zilivyo katika aya ya 8(iii) na (v) za kiapo kwa pamoja kuhusu Tume kuegemea nyaraka ambayo haikuwahi kutolewa kama kielelezo katika kufiikia uamuzi wake. Nyaraka hiyo ni Kanuni za Watumishi wa Shirika la Maendeleo Dar es salaam (Dar es salaam Development Corporation staff Regulations). Kwakuwa Tume iliegemea uamuzi wake katika nyaraka hiyo ni maoni ya Mleta Maombi kuwa nyaraka ilitolewa mbele ya Tume bila waleta maombi kuwepo. Suala kama hili liliamuliwa na Mahakama ya Rufaa katika kesi ya **Bayport Financial Services (T) Ltd dhidi ya Cresence Mwandele,** Rufaa ya muda Na. 19 ya 2017, Mahakama ya Rufaa Tanzania iliyoko Mbeya, (haijaripotiwa), ambapo Mahakama ya Rufaa iliamua kwamba wasuluhishi na waamuzi hawaruhusiwi kukutana na mdaawa mmoja bila mwingine kuwepo kwa mujibu wa kanuni ya 5(i) ya Tangazo la Serikali Na. 66 la 2007. Na Mahakama kuu Divisheni ya Kazi inaweza kufuta Tuzo iliyotolewa na Tume iwapo kutakuwa na mwenendo usiofaa wa muamuzi.

Shahidi wa Mjibu Maombi hakueleza katika ushahidi wake kuwa Kanuni hizo za Watumishi wa Shirika la Maendeleo Dar Es Salaam zinatekelezwa chini ya Sheria ipi. Aidha, hakuna kanuni au Sheria inayosema kuwa kanuni hizo zitatumika pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma. Kifungu cha 12 cha kanuni hizo za watumishi wa Shirika kinaeleza kuwa kanuni hizo zitatumika pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma pamoja na kanuni zenyewe lakini Tume iliamua kuwa mleta maombi ameachishwa kazi kihalali kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

Hoja ya mwisho iliyowasilishwa na Wakili wa Mleta Maombi ni hoja ya kisheria ya 8 ambayo inapatikana katika aya ya 8(vi) ya kiapo cha mleta maombi kuwa mleta maombi hawezi kuwa mtumishi wa Umma wakati shirika la Maendeleo Dar es salaam- DDC liliondolewa katika orodha ya Mashirika ya Umma mwaka 1992, na kifungu cha 30 cha Sheria ya mashirika ya Umma ya 1992. Sheria ilieleza kuwa mashirika yaliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mashirika ya Maendeo ya Wilaya yatakoma kuwa mashirika ya Umma. Kwa sababu hiyo mleta maombi hana sifa ya kuwa Mtumishi wa Umma na hata uwepo wa mjibu maombi sio halali kwa mujibu wa sheria. Hivyo anaomba Mahakama ifanyie marejeo uamuzi wa Tume, ifute uamuzi wa Tume na kutoa amri ya kusikilizwa kwa mgogoro huu kwa kuwa Tume inayo mamlaka ya kuusikiliza.

Akijibu mawasilisho ya wakili wa Mleta Maombi, wakili wa Mjibu Maombi ameeleza akijibu hoja ya kwanza kuwa shirika la maendeleo ya Dar es salaam sio shirika la Umma. Aya ya 5 ya kiapo kinzani imeeleza kuwa Mjibu Maombi ni Taasisi ya Umma ambayo imeanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha Sheria ya Mashirika ya Wilaya sura ya 382 kama ilivyorejewa mwaka 2002 ( The District Development Corporations-Act, Cap. 382 R.E. 2002). Kiapo kinzani kimeeleza kuwa shirika lipo chini ya Bodi ya Wakurugenzi ambapo mwenyekiti wa Bodi huteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wajumbe wengine huteuliwa na Waziri husika wa serikali za mitaa kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam. Tangazo la Serikali Na.13 la Mwaka 2000 linaonesha kuwa mlalamikiwa alikuwa chini ya jiji la Dar es salaam. Kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika ya Maendeleo ya Wilaya kifungu cha 7(5) imeipa mamlaka Bodi ya shirika kutengeneza kanuni za watumishi. Hivyo waajiriwa wote wa mjibu maombi ni watumishi wa Umma na wapo chini ya usimamizi wa sheria iliyoanzisha Shirika, kanuni zake pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma na kanuni zake.

Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma ya 2007 kupitia Sheria ya marekebisho ya Sheria Na.18 ya mwaka 2007 imeongeza kifungu cha 31(2) katika Sheria ya Utumishi wa Umma, sura ya 18, kama ilivyorejewa mwaka 2019. Kifungu hicho cha 31(1) kinasema watumishi

walio katika wakala za Serikali na Taasisi za serikali zitakuwa chini ya sheria inazozianzisha. Kifungu kidogo cha pili (2) cha kifungu cha 31 inaeleza kuwa watumishi hao pia watakuwa chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

Wakili ameeleza kuwa baada ya mabadiliko hayo serikali ilitoa waraka wa tarehe 12/05/2008 wenye Kumb. Na. UTUMISHI Kumb. C/AC/45/257/101/C/99 ikieleza utekelezaji wa mabadiliko ya sheria kuhusiana na watumishi walio katika wakala za serikali na Taasisi za Umma. Taasisi na wakala hizo zilitakiwa kuwa chini ya sheria inazozianzisha na pia chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma na kama kutakuwa na mgogoro kati ya Sheria hizo na Sheria ya Utumishi wa Umma basi Sheria ya Utumishi wa Umma ndiyo itapewa kipaumbele. Mwaka 2015 kulifanyika Marekebisho ya Sheria za kazi kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria za kazi Na. 24 ya 2015 ambayo iliongeza kifungu cha 32A katika Sheria ya Utumishi wa Umma. Nyongeza hii ilieleza kwamba kama kutakuwa na mgogoro baina ya Sheria zinazoongoza Taasisi za Umma na Sheria ya Utumishi wa Umma basi Sheria ya Utumishi wa Umma ndio itakayofuatwa na kupewa uzito.

Msimamo huu wa kisheria ulirejewa na Mahakama kuu katika kesi ya **Meshack L.N. Kegya dhidi ya Shirika la Petroli Tanzania**, mgogoro wa kazi Na. 4 wa 2018, Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi,

iliyoketi Dar Es Salaam, (haijaripotiwa), ambapo Mahakama iliamua kuwa Watumishi wa Taasisi za Umma wataongozwa na Sheria zinazoongoza Utumishi wa Umma. Na pale kutakapokuwa na mgogoro kati ya Sheria hizo Sheria ya Utumishi wa Umma ndio itakayofuatwa kwa mujibu wa kifungu cha 22 cha Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Ajira na Sheria za kazi ya mwaka 2015.

Wakili aliendelea kueleza kuwa Mleta maombi katika shauri hili alikuwa mwajiriwa wa Mjibu Maombi. Watumishi wote wa Mjibu Maombi wanaongozwa na Sheria iliyoanzisha Shirika na Sheria ya Utumishi wa Umma pamoja na kanuni zake. Sheria ya Utumishi wa Umma inatambua kuwa Afisa Masuhuli Mkuu ndiye mwenye mamlaka ya nidhamu ya Waajiriwa wote. Kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika ya Maendeleo ya Wilaya ni Meneja mkuu wa shirika na ndiye atawajibika kwa Bodi ya wakurugenzi ya shirika kuhusu uendeshaji wa shirika. Sheria ya Utumishi wa Umma, imeeleza kuwa mamlaka ya nidhamu kwa mtu au mamlaka yoyote iliyopewa nguvu katika Sheria ya Utumishi wa Umma kuchukua hatua za nidhamu dhidi ya watumishi wake. Kifungu cha 4(3) (d) na 31(2) cha Sheria hiyo vikisomwa pamoja na kanuni ya 35(2) (b) ya Kanuni za Utumishi wa Umma inasema kiongozi Mkuu wa Taasisi ya Umma inayojitegemea ndiye atakuwa na mamlaka ya nidhamu ya watumishi walio chini yake.

Wakili wa Mjibu Maombi alitafsiri Idara Huru ya Taasisi ya Umma kwa kutumia kanuni ya 3 ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya 2003 kuwa in idara inayojitegemea ambayo haipo moja kwa moja chini ya Wizara. Aidha, Mjibu Maombi ni taasisi ya Serikali inayojitegemea iliyoundwa kwa Sheria ya Mashirika ya Maendeleo ya Wilaya na iko chini ya Bodi ya Wakurugenzi na hivyo Meneja Mkuu ni mamlaka sahihi ya Nidhamu ya Watumishi walio chini yake. Kiongozi Mkuu wa Taasisi pia anatambulika na kanuni za kudumu za Utumishi wa Umma (Standing Orders for Public Service) kanuni ya A.1 katika aya ya 8. Baada ya kuachishwa kazi na mkuu wa taasisi, Mleta Maombi alipaswa kufuata taratibu za Watumishi wa Umma kama zilivyo katika Sheria ya Utumishi wa Umma. Mamlaka ya Rufaa kwa Mleta Maombi kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma ni Tume ya Utumishi wa Umma. Hii ni mujibu wa kifungu cha 9(3)(e),25(1)(b) na31(2) cha Sheria ya Utumishi wa Umma zikisomwa pamoja na kanuni ya 60(2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2003. Sheria na kanuni zinaeleza kuwa maamuzi ya wakuu wa Taasisi yanakatiwa Rufaa kwenda Tume ya Utumishi wa Umma.

Mleta maombi wakati anawasilisha shauri Tume ya Usuluhishi na Uamuzi hakuwa amefuata taratibu za Rufaa kama kifungu cha 32A cha Sheria ya Utumishi wa Umma kinavyoeleza kuwa akamilishe kwanza taratibu zilizopo ndani ya Sheria kabla ya kutafuta haki yake katika

vyombo vingine vya kisheria. Mahakama hii ilikuwa na msimamo sawa na huo katika shauri la **Faima Siraji dhidi ya Mamlaka ya maji Safi na maji Taka Mbeya**, marejeo ya kazi Na. 47 ya 2017 Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi, Mbeya (haijaripotiwa), ambapo Mahakama iliamua kuwa Mtumishi wa Umma anatakiwa kufuata taratibu za ndani kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma kabla ya kufuata taratibu za Sheria nyingine. Mleta Maombi hajafuata taratibu, hivyo Tume ilikuwa sahihi kuufutilia mbali mgogoro uliokuwa umewasilishwa mbele yake.

Kuhusiana na hoja ya Mleta Maombi kuwa Sheria ya Mashirika ya Umma iliyafuta Mashirika ya Maendeleo ya Wilaya kuwa Mashirika ya Umma, wakili wa Mjibu Maombi alieleza kuwa Sheria ya Mashirika ya Umma iliyaondoa Mashirika ya Maendeleo ya Wilaya kwenye tafsiri ya Mashirika ya Umma kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha Sheria hiyo. Kesi ya **Floriana Kinawiro** iliyonukuliwa na mleta maombi ilifunguliwa mwaka 2012 na hukumu kutolewa tarehe 26/01/2016 kabla ya mabadiliko ya sheria ya Utumishi wa Umma kupitia Sheria ya mabadiliko ya Sheria Na. 3 ya 2016. Hivyo kesi hiyo ni tofauti na kesi ya sasa kwa kuwa Sheria imebadilika na sasa Sheria ya Utumishi wa Umma inataka Mtumishi kumaliza taratibu za ndani za utatuzi wa migogoro ya kazi kabla ya kufuata taratibu za sheria nyingine. Naomba kesi hiyo isizingatiwe.

Wakili wa Mjibu Maombi akijibu kuhusu tafsiri iliyotolewa na Mleta Maombi kuwa watumishi wa mlalamikiwa wameondolewa katika Utumishi wa Umma wanaoongozwa na Sheria hiyo kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma katika kifungu cha 3(a) ameeleza kuwa tafsiri hiyo si sahihi. Tafsiri sahihi ya kifungu hicho ni kuwa Watumishi wa Umma ni Watumishi wote wanaofanya kazi katika ofisi ya Umma. Na ofisi ya Umma ni ofisi yoyote ya Umma katika Jamhuri ya muungano wa Tanzania ambayo imepewa jukumu la kutunga sera za serikali au kutoa huduma kwa Umma. Ofisi za Umma ambazo watumishi wake hawapo chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma ni watumishi wa Bunge, wajumbe wa mabaraza, bodi, kamati, au vikundi au vyombo vya namna hiyo ambavyo huenda au la vimeanzishwa kwa sheria, ofisi ya Jaji au watumishi wa Mahakama, Jeshi la polisi au Magereza au watumishi wanaolipwa kwa masaa, kwa siku au mkataba wa kipindi maalum. Tafsiri iliyopo haimuhusu kabisa mleta maombi kwani siyo sehemu ya vyombo au ofisi hizo.

Wakili aliitofautisha kesi ya **Jeremiah Mwandi dhidi ya shirika la posta Tanzania** iliyonukuliwa na mleta maombi na shauri hili kuwa Mahakama ilichukulia Shirika la Posta ni Shirika la Umma lenye Watumishi wake na liliona kuwa kabla ya kuendesha kesi mleta maombi katika kesi hiyo alikuwa Mtumishi wa Umma. Shauri hili halikuonyesha mabadiliko ya sheria ya waka 2007. Hivyo maamuzi yalifikiwa bila kuzingatia Sheria,

Kanuni za Huduma za Utumishi wa Umma katika kanuni 4.1 aya ya 52 inaeleza kuwa Utumishi wa Umma ni mfumo wa Taasisi iliyopewa jukumu la utoaji wa huduma kwa Umma kama ambavyo Umma unategemea kutoka kwa Shirika au Taasisi yoyote kwa niaba ya serikali.

Kuhusu madai ya Mleta Maombi kuwa Mtumishi wa Umma hupimwa kwa kuangalia ngazi ya mshahara kwa mfano TGS au "check Namba" alieleza kuwa hicho sio kipimo cha kumtambua Mtumishi wa Uma bali sheria ndio inasema nani ni Mtumishi wa Umma.

Kuhusu Maelezo ya Mleta Maombi kwa Mjibu Maombi alikutana na mwamuzi bila kuwepo upande wa Mleta Maombi, wakili wa Mjibu Maombi ameeleza kuwa maelezo hayo yametolewa kwa mara ya kwanza wakati wa kuwasilisha maelezo yao. Maelezo hayo sio sehemu ya kiapo cha mleta maombi. Hivyo anaomba yasipokelewe kwa kuwa wadaawa wanafungwa na maelezo yao waliyowasilisha mbele ya Mahakama. Mahakama ya Rufaa illikuwa na msimamo kama huo katika kesi ya **Linus Chengula dhidi ya Frank nyika**, Rufaa ya madai Na. 131 ya 2015, Mahakama ya Rufaa Tanzania, iliyoketi Iringa. Sio kweli kwamba Mjibu Maombi alikutana ma muamuzi bila Mleta Maombi kuwepo. Kanuni za Watumishi wa mjibu maombi zilitolewa wakati wa majumuisho, hivyo, hoja ya Mleta Maombi haina mashiko. Kesi ya **Bayport** iliyonukuliwa na mleta maombi ina mazingira tofauti na kesi hii na naomba Mahakama

isiipe uzito wowote kwa kuwa katika kesi hiyo muamuzi alikutana na upande mmoja bila upande mwingine kuwepo na kuongeza muda wa kuwasilisha majumuisho ya mwisho. Hivyo Tume ilikuwa sahihi kulinda shauri hili.

Akifanya Mawasilisho ya nyongeza (Rejoinder submission), Wakili wa Mleta Maombi alieleza kuwa Kesi ya **Faima Siraji na kesi ya Meshack L.N. Kagya** ambazo zimenukuliwa na Mjibu Maombi ni tofauti na kesi iliyo mbele yetu. Wadaiwa katika kesi hizi walikuwa ni Watumishi wa Taasisi za Umma zenye majukumu ya moja kwa moja ya kutekeleza shughuli za kiserikali. Mleta maombi hahusiki kutekeleza shughuli za kiserikali hivyo kesi hizo haziwezi kutumika. Mtumishi wa Umma tafsiri yake inatolewa na Sheria ya Utumishi wa Umma. Sifa za Mleta Maombi kama Mtumishi wa Umma zipo mbali mno katika Sheria ya Utumishi wa Umma.

Kutokana na mawasilisho yaliyotolewa na pande zote mbili, Mleta Maombi ameeleza kuwa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi ilikosea kuona kuwa Mleta Maombi ni Mtumishi wa Umma hivyo alitakiwa akamilishe taratibu za ndani zilizowekwa na Sheria ya Utumishi wa Umma kabla ya kupeleka mgogoro wake mbele ya Tume na hivyo kutoa uamuzi kuwa haikuwa na mamlaka ya kusikiliza mgogoro huo uliowasilishwa mbele yake. Mleta Maombi katika maelezo yake ameeleza kuwa yeye sio

Mtumishi wa Umma kwa sababu Mjibu Maombi anamilikiwa na Halmashauri ya Jiji, Mjibu Maombi anaongozwa na Bodi ya Wakurugenzi, Mleta Maombi alikuwa ameajiriwa na alikuwa akilipwa mshahara wake na Bodi ya Shirika, hakuwa na namba ya cheki na mshahara wake haukuwa katika ngazi za TGS kama watumishi wengine wa Umma. Pia alieleza kuwa Shirika la Maendeleo Dar Es Salaam – DDC liliondolewa na kifungu cha 30 cha Sheria ya Mashirika ya Umma kuwa miongoni mwa Mashirika ya Umma. Akijibu hoja hizo, Mjibu Maombi katika mawasilisho yake alieleza kuwa Shirika la Maendeleo Dar Es Salaam - DDC ni Taasisi ya Umma ambayo imeanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha Sheria ya Mashirika ya Wilaya sura ya 382 ya sheria kama ilivyorejewa mwaka 2002 (The District Development Corporations - Act, Cap. 382 R.E. 2002). Kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika ya Maendeleo ya Wilaya kifungu cha 7(5) kimeipa mamlaka Bodi ya shirika kutengeneza kanuni za watumishi. Kanuni zilizotengenezwa na Bodi zinaeleza kuwa Kanuni hizo zitatumika pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma katika masuala ya kiutumishi ya watumishi wa shirika. Hivyo waajiriwa wote wa Mjibu Maombi ni watumishi wa Umma na wapo chini ya usimamizi wa sheria iliyoanzisha Shirika, kanuni zake pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma na kanuni zake.

Ni maoni yangu kuwa tafsiri ya nani ni Mtumishi wa Umma ni suala la kisheria. Kwa tafsiri ya Sheria ya Utumishi wa Umma ya 2002, Mtumishi wa Umma kwa madhumuni ya sheria hiyo ni mtu aliye au anayefanya kazi katika Ofisi ya huduma kwa Umma. Na Ofisi ya huduma kwa Umma kwa madhumuni ya Sheria ya Utumishi wa Umma imetafsiriwa na kifungu cha 3(a) (i) (ii) (iii) (iv) (v), na 3(b) kuwa ni Ofisi ya Umma katika Jamhuri ya Muungano ambayo inalipwa kwa kufanya kazi ya kuandaa sera za Serikali na kutoa huduma kwa umma ambazo sio ofisi ya Bunge, Ofisi ya mjumbe wa Baraza, Bodi, Timu, Kamati au chombo kinachofanana navyo iwe ni shirika lililoanzishwa kwa au chini ya sheria yoyote, ofisi ambayo malipo yake yanalipwa kwa masaa, kwa siku au kipindi cha mkataba, ofisi ya Jaji au ofisi ya Mahakama, Ofisi katika Jeshi la Polisi au Huduma ya Magereza. Kutokana na tafsiri hii ni wazi kuwa kuna ofisi za huduma kwa umma ambazo hazisimamiwi na Sheria ya Utumishi wa Umma kama ilivyo ilivyoelezwa na Mahakama hii katika kesi ya **Jeremiah Mwandi dhidi ya Shirika la Posta Tanzania, Marejeo Na. 06 ya 2019, Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi, iliyoketi Kigoma.**

Aidha, Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma katika Kanuni A.1 (52) inatoa tafsiri ya Utumishi wa Umma kuwa ni mfumo au asasi iliyokabidhiwa wajibu wa kutoa au kusimamia utoaji wa huduma zinazohitajiwa na Umma kutoka Serikalini au taasisi nyingine yeyote

inayotua huduma kwa niaba ya Serikali kwa mujibu wa Sheria. Maelezo ya Mjibu Maombi yanaonesha kuwa DDC inatoa huduma kwa Jamii kwa kuelekezwa moja kwa moja na Halmashauri ya Jiji la Dar Es Salaam na pia huwa inatoa gawio kwa jiji ili kuwezesha huduma za kijamii kufanyika ipasavyo.

Sheria ya Utumishi wa Umma inasimamia watumishi wa Umma wengine wote ambao ni watumishi wa Serikali au wanaotoa huduma kwa niaba ya Serikali katika taasisi zake kasoro kwa watumishi wa umma wanaofanya kazi katika ofisi za umma zinazotajwa katika kifungu cha 3(a) (i) (ii) (iii) (iv) na (v). Swali la kujiuliza ni je Mjibu Maombi ni Ofisi ya Umma? Sheria ya Mashirika ya Wilaya, Sura ya 382 Kama ilivyorejewa 2002, katika kifungu cha 2(1) (a) na (b) inatafsiri Shirika la Maendeleo ya Wilaya ni Kampuni yoyote iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni kwa ajili ya kufanya biashara ya aina yoyote katika eneo la Serikali za Mitaa ambalo mtaji wake au sehemu ya mtaji wake umewekezwa na Mamlaka ya Serikali za Mtaa au Menejimenti yake imekasimishwa kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Sheria hiyo pia inatafsiri Shirika la Wilaya kuwa ni shirika la umma lililoanzishwa katika wilaya yoyote au wilaya mbili au zaidi kwa amri itakayotolewa na Waziri mwenye mamlaka na tawala za mikoa. Shirika hili lilianzishwa mwaka 1971 na mwaka 1973 liliwekwa chini ya Sheria ya Mashirika ya Maendeleo ya Wilaya. Maelezo yanaonesha kuwa

Mjibu Maombi alianzishwa kwa amri ya Waziri mwenye dhamana ya tawala za mikoa kwa tangazo la serikali.

Swali la msingi la kujiuliza ni kuwa taasisi ya umma inaweza kumiliki kampuni ambayo sio ya umma? Ni maoni yangu kuwa jibu ni hapana. Kama Shirika linamilikiwa na Taasisi ya umma ambayo ndiyo yenye asilimia kubwa ya umiliki wa hisa au mtaji maana yake shirika hilo ni mali ya umma na linatoa huduma zake kwa umma. Hivyo, Mjibu Maombi ni shirika la umma hata kama sio miongoni mwa mashirika ya umma yanayosimamiwa chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma. Na ushahidi uliopo unaonesha kuwa Mleta Maombi alikuwa ni mtumishi wa Mjibu Maombi. Hivyo Mjibu Maombi sio miongoni mwa Ofisi za zinazotoa huduma kwa umma zinazo tenganishwa na kifungu cha 3(1) (a) cha Sheria ya Utumishi wa Umma.

Tume ya Usuluhishi na Uamuzi iliamua katika mgogoro uliokuwa mbele yake kuwa Tume haijakatazwa kusikiliza mashauri ya watumishi wa Umma, ila inakatazwa kusikiliza mashauri ya watumishi wa Umma kabla hawajakamilisha taratibu za utumishi wa Umma kabla ya kwenda Tume. Tume iliona kuwa Mleta Maombi alikuwa ni Mtumishi wa Umma hivyo alitakiwa akamilishe taratibu za ndani zinazowekwa na Sheria ya Utumishi wa Umma kabla ya kufungua Mgogoro mbele ya Tume. Katika kufikia

uamuzi huo Tume iliona kuwa Kanuni za Watumishi wa DDC katika Kipengele cha 12.0 kuhusu Kuacha kazi inayopatikana katika ukurasa wa 44 inaeleza wazi kuwa mtu anapoachishwa kazi Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma zitatumika pamoja na Kanuni za Watumishi wa DDC. Taratibu husika ni kuwa Mtumishi akiachishwa kazi na Bodi ya Wakurugenzi anatakiwa akate Rufaa kwa Waziri. Pamoja na kuwa rekodi za Tume hazioneshi namna kanuni hizo za watumishi wa DDC zilitolewa mbele ya Tume au namna Tume ilivyozipata, lakini bado maelezo yaliyopo katika rekodi yanathibitisha kuwa Mjibu Maombi ni Ofisi ya Huduma kwa Umma inayomilikiwa na Halmashauri ya jiji la Dar Es Salaam.

Mleta Maombi ameeleza kuwa Mjibu Maombi aliondolewa katika orodha ya Mashirika ya Umma na kifungu cha 30 cha Sheria ya mashirika ya Umma ya 1992. Sheria ilieleza kuwa mashirika yaliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mashirika ya Maendeo ya Wilaya yatakoma kuwa mashirika ya Umma. Ni kweli kifungu hicho cha 30 kimeondoa Mashirika ya Maendeleo ya Wilaya kuwa Mashirika ya Umma kuanzia mwaka 1992 sheria hiyo ilipoanza kufanya kazi. Lakini ni Maoni yangu kuwa kuondolewa kwa Mjibu Maombi kuwa Shirika la Umma hakufanyi Mjibu Maombi asiwe ni Ofisi ya Huduma za Umma (Public Service Office). Hivyo ni maoni yangu kuwa Mjibu Maombi ni Ofisi ya Huduma za Umma na Mleta Maombi ni Mtumishi wa Umma anayefanyia kazi katika Ofisi hiyo ya Umma.

Baada ya kuona kuwa mleta maombi ni Mtumishi wa Umma, swali linalofuata ni iwapo Mleta Maombi ni Mtumishi wa Umma kwa madhumuni ya Sheria ya Utumishi wa Umma. Kama nilivyoeleza hapo juu, Sheria ya Utumishi wa Umma katika kifungu cha 3 (a) na (b) inatambua kuwa ofisi yoyote ile inayotunga sera za Serikali, kutoa huduma kwa Umma kuwa ni ofisi ya huduma kwa Umma isipokuwa ofisi ya Bunge, Ofisi ya mjumbe wa Baraza, Bodi, Timu, Kamati au chombo kinachofanana navyo iwe ni shirika lililoanzishwa kwa au chini ya sheria yoyote, ofisi ambayo malipo yake yanalipwa kwa masaa, kwa siku au kipindi cha mkataba, ofisi ya Jaji au ofisi ya Mahakama, Ofisi katika Jeshi la Polisi au Huduma ya Magereza. Ofisi ya Huduma kwa Umma pia ni ofisi yeyote inayotamkwa na sheria yoyote au chini ya sheria yoyote kuwa ofisi ya umma. Ni wazi kuwa Sheria ya Mashirika ya Maendeleo ya Wilaya inaeleza kuwa Mashirika hayo ni ya Umma amabayo yatasimamiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Na Ushahidi unaonesha kuwa Shirika la Maendeleo ya Dar Es Salaam linamilikiwa na kusimamiwa na Halmashauri ya Jiji la Dar Es Salaam kupitia bodi ya wakurugenzi. Shughuli za shirika hilo ni kutoa huduma mbalimbali kwa umma kwa njia ya kufanya biashara. Hakuna maelezo au ushahidi wowote katika rekodi ambao unaonesha kuwa Mjibu Maombi anamilikiwa na mtu au taasisi nyingine ambayo sio ya umma. Maelezo ya

Mleta Maombi kuwa Mjibu Maombi kuwa hayupo kihalali ni wa kushangaza kwa kuwa ni sawa na kusema anashitaki shirika ambalo halipo.

Kuhusu kesi ya **Jeremiah Mwandi dhidi ya Shirika la Posta Tanzania** ambayo imenukuliwa na Mleta Maombi, kesi hiyo haifanani na kesi iliyo mbele yetu kwa kuwa kesi hii Mjibu Maombi anamilikiwa na Halmashauri ya Jiji la Dar Es Salaam ambayo ni Mamlaka ya Serikali za Mitaa inayotoa huduma kwa UMMA. Hivyo, ni maoni yangu kuwa Mjibu Maombi anamilikiwa na Halmashauri ya Jiji la Dar Es Salaam na Mleta Maombi ni Mtumishi wa Umma anayetakiwa kufuata Sheria ya Utumishi wa Umma.

Kwa kuwa nimeona Mleta Maombi ni Mtumishi wa Umma kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, kifungu cha 32A cha Sheria ya Utumishi wa Umma kinamtaka Mtumishi wa Umma aliyeachishwa kazi kukamilisha taratibu za kupata nafuu zilizowekwa na Sheria hiyo kabla ya kutafuta nafuu katika sheria za kazi. Mjibu maombi ameeleza kuwa Mleta Maombi alitakiwa akate rufaa kwenda kwa Tume ya Utumishi wa Umma. Mleta Maombi hajaeleza kama alikata rufaa kwenda kwa Tume ya Utumishi wa Umma hivyo ni wazi kuwa hakufuata taratibu zilizowekwa na Sheria ya Utumishi wa Umma. Hivyo nakubaliana na uamuzi wa Tume wa

kuwa mgogoro husika ulifikishwa mapema kabla ya kukamilisha taratibu za rufaa kwa mujiba wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

Kwa sababu hiyo, naona kuwa shauri hili halina mashiko na hivyo nalitupilia mbali (dismiss). Kila upande utajigharamia gharama za uendeshaji wa shauri hili.

**A. E. MWIPOPO**
**JAJI**
**07/05/2021**